JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA AROBAINI

**10 JUNI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA AROBAINI – 10 JUNI, 2016

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/2017 – 2020/2021 (*The Second National Five Year Development Plan, 2016/2017 – 2020/2021).*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## II. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 334. MHESHIMIWA MARTHA JACHI UMBULLA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kamati za Fedha na Mipango za Halmashauri za Wilaya ni Kamati muhimu sana kwa Wabunge wote kushiriki bila kujali ni Mbunge wa Viti Maalum au wa Jimbo kwa sababu zinashughulika na masuala ya fedha, bajeti na mipango ya miradi ya maendeleo; na kwa muda mrefu sasa Wabunge wa Viti Maalum wamekuwa wakiomba kuondolewa kwa Sheria kandamizi na ya kibaguzi ya kuwazuia kushiriki katika Kamati hizo:-

(a) Je, Serikali iko tayari kusikiliza kilio hicho cha Wabunge wa Viti Maalum ili kuwaruhusu kushiriki kwenye Kamati hizo;

(b) Je, Serikali iko tayari kufuta Sheria hiyo kandamizi na yenye ubaguzi ambayo haina tija na hasa ikizingatiwa kuwa ilitungwa mwaka 1998 wakati ambao Ubunge wa Viti Maalum ulikuwa bado haujaanza.

**335. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kutoka Kijiji cha Mutelewele kwenda Makambako ni km 5 wakati kwenda Halmashauri ya Wanging'ombe ni km 65; Kutoka Kata ya Soja kuja Makambako mjini ni km 25 na kwenda Halmashauri yao ya Wanging'ombe ni km 88; na kutoka Kijiji cha Nyigo kuja Makambako ni km 8 wakati kwenda Halmashauri ya Mufindi ni km 88 na huduma zote zikiwemo matibabu wanazipata Makambako; kutoka Kijiji cha Igongolo ni umbali wa km 6 kwenda Makambako wakati kwenda Halmashauri ya Njombe ni km 54:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kugawa mipaka upya ili Wananchi wapate huduma karibu na Halmashauri yao ili iendane na kaulimbiu ya kusogeza huduma karibu na Wananchi;

(b) Je, ni lini sasa Serikali itapima upya mipaka hiyo.

**336. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali ilikwishaanza kujenga vituo vya afya katika Vijiji vya Mima na Mbori; na ujenzi huo umesimama kutokana na ukosefu wa fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa vituo hivyo ili Wananchi wa maeneo hayo wapate huduma za afya.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**337. MHESHIMIWA HALIMA ALI MOHAMED (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Serikali imejipanga kupiga vita suala la ajira kwa watoto na imekuwa ikiunga mkono matamko ya Umoja wa Mataifa kuhusiana na ajira za watoto:-

Je, kupitia mradi wa TASAF III Serikali ina mikakati gani ya makusudi kuwasaidia watoto na tatizo la ajira za utotoni kwa upande wa Zanzibar.

## WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

**338. MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA (RUFIJI)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Wakulima wa zao la Korosho katika Jimbo la Rufiji wameibiwa zaidi ya Sh. 900,000,000/= kwa mwaka 2011 kutoka kwa vyama vya msingi vya Kimani, Mwasani, Kibiti na Ikwiriri:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua kali dhidi ya vyama hivyo.

**339. MHESHIMIWA JEROME DISMAS BWANAUSI (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Serikali iliwaahidi Wakulima wa Korosho kupata malipo halali ya mauzo ya Korosho kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani:-

(a) Je, ni lini Serikali itawahakikishia Wakulima wa Korosho wa Wilaya ya Masasi kuwa watalipwa malipo yao ya mwisho wanayostahili;

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa Vyama vya Ushirika ambavyo haviwalipi Wakulima wa Korosho fedha zao kama Korosho zilivyouzwa kwenye mnada.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**340. MHESHIMIWA JAMES KINYASI MILLYA (SIMANJIRO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Tangu kuanzishwa kwake Wilaya ya Simanjiro haijawahi kupata maji ya uhakika, licha ya ahadi mbalimbali ikiwemo ile ya Rais wa Awamu ya Nne kuwa Simanjiro itatengewa bilioni 30 ili kuleta maji kutoka Mto Ruvu hadi Makao Makuu ya Wilaya Orkesumet:-

Je, Serikali itatekeleza lini ahadi hiyo ili kuwakomboa Wananchi wa Simanjiro.

**341. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Miradi ya kuboresha huduma ya maji inayofadhiliwa na Benki ya Kiarabu (BADEA), Shirika la Mafuta Ulimwenguni (OFID) na Serikali ya Tanzania katika Kijiji cha Mwankoko na Kisaki katika eneo la IRAO inaleta changamoto kubwa:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kulipa fidia kwa Wananchi waliopisha miradi hiyo ambapo tayari uthamini ulishafanyika kwa mara ya pili ambapo Mwankoko wanadai Tshs.1,510,427,634 na uthamini ulifanyika 13 Machi, 2014 mradi wa IRAO Tshs.2,932,001,058/=;

(b) Mradi wa maji wa IRAO katika visima vyake vyote viwili vinapoteza uwezo wa kutoa maji kutoka Q250-170 kwa saa na kisima cha pili ni Q150-70 kwa saa; Je, Serikali ina mpango gani juu ya kukabiliana na tatizo hilo.

**342. MHESHIMIWA SUSAN LIMBWENI KIWANGA (MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Pamoja na Jimbo la Mlimba kuwa na vyanzo vingi vya maji ikiwemo mito mikubwa Wananchi bado wanakumbwa na uhaba mkubwa na maji safi na salama:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha mpango wa usambazaji wa maji safi na salama kwa Wananchi wa Mlimba;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha skimu za umwagiliaji ili kuvipa tija vyanzo vya maji vilivyopo katika Jimbo la Mlimba.

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

**343. MHESHIMIWA KANYASU CONSTANTINE JOHN (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Mgodi wa GGM – Geita umepewa eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 192 kwa ajili ya kuchimba Dhahabu wakati Wananchi wamenyang’anywa maeneo yao:-

Je, ni lini maeneo yaliyonyang’anywa Wananchi yatarudishwa kwa Wananchi.

## III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2016 *(The Finance Bill, 2016).*

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**10 JUNI, 2016** **KATIBU WA BUNGE**